



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



**Kumb. Na. HW/ITG/F2/6/ 55**

**15 Octoba, 2024.**

**WANANCHI WOTE,**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI.**

## **Yah: TANGAZO LA KAZI ZA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa nafasi za kazi (11) za wafanya usafi wa Mazingira na Udhhibiti wa Taka. Waombaji wa nafasi hizo wawasilishe maombi yao ya kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itigi kwa kuzingatia vigezo na maelekezo kama ilivyo katika tangazo hili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi 11 za ajira ya mkataba kwa kazi ya kufanya usafi na Udhhibiti wa taka. Nafasi za kazi zinazotangazwa ni zifuatazo:-

### **1.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

- ❖ Awe raia wa Tanzania
- ❖ Awe na umri kati ya miaka 18 na 65
- ❖ Awe na elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea
- ❖ Awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kishwahili
- ❖ Awe mwenye afya njema
- ❖ Awe mchapakazi na mwenye kujituma
- ❖ Awe mwenye nidhamu ya kazi
- ❖ Awe na utayari wa kufanya kazi kwa muda usiopungua masaa nane(8) kwa siku
- ❖ Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

## 1.2 MAJUKUMU YA KIBARUA WA USAFI

Kufanya usafi wa mazingira ya maeneo yafuatayo:-

- I. Stendi ya mabasi ya Itigi na Rungwa
- II. Nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri
- III. Maeneo ya wazi
- IV. Maeneo ya dampo
- V. Maeneo ya utawala
- VI. Maeneo ya Barabara kuu
- VII. Maeneo ya minada
- VIII. Maeneo ya machinjio Itigi na Mitundu
- IX. Kazi nyingine zote zitakazopangwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Itigi

## 1.3 UTARATIBU WA MALIPO

Kibarua wa usafi wa ajira ya Mkataba atalipwa kulingana na mkataba atakaolingia na Halmashauri.

Maombi yote ya kazi yatumwe kwanzia tarehe 21/10/2024 hadi 28/10/2024 kwa Anuani ifuatayo;

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi  
01 BR. YA HALMASHAURI  
S.L.P. 70  
43483 ITIGI- SINGIDA

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA :**

Ayoub J. Kambi  
**MKURUGENZI MTENDAJI(W)e**



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,  
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi